ANZA SAFARI YA KUJIFUNZA

# Nadharia Ya Muziki

## HATUA YA KWANZA



*Mwongozo wa Mwalimu na Mwanafunzi kwa Mafunzo ya Muziki Hatua ya Kwanza*

**WILLIAM MICHAEL KASENGA**

# ANZA SAFARI YA KUJIFUNZA

# NADHARIA YA MUZIKI

HATUA YA KWANZA

*Mwongozo wa Mwalimu na Mwanafunzi kwa Mafunzo*

*ya Muziki Hatua ya Kwanza*





**WILLIAM MICHAEL KASENGA**

©2025

**WILLIAM MICHAEL KASENGA**

Simu: +255 753 239 953 / +255 717 523 355
Baruapepe: kasenga66@gmail.com

**HAKI ZOTE ZIMEHIFADHIWA!**

*Hairuhusiwi kutoa nakala sehemu yoyote ya kitabu hiki kwa namna yoyote bila idhini ya mmiliki wa kitabu hiki, isipokuwa kwa kunukuu kuliko ruhusiwa kisheria.*

**ISBN: 978_9912_42_949_9**

**Sanifu Ya Jalada na Kurasa (Book Cover Design & Typesetting) imefanywa Na:**
Lamax Designs, +255 764 793 105
lamaxdesigns@gmail.com

**MHARIRI:** Peter Simon Haule | +255 713 140 303

# YALIYOMO

WAKFU MAALUM ---------- iv

SHUKRANI ---------- v

UTANGULIZI ---------- vii

Sura Ya Kwanza: MAANA YA MUZIKI ---------- 1

Sura Ya Pili: ALA ZA MUZIKI ---------- 10

Sura Ya Tatu: MAUMBO YA NOTA ---------- 15

Sura Ya Nne: ALAMA NYEPESI ZA WAKATI ---------- 25

Sura Ya Tano: STAFU NA VITAMBULISHO VYA SAUTI ---------- 42

Sura Ya Sita: NGAZI KUU ZA C, G, D na F ---------- 66

Sura Ya Saba: MSAMIATI ---------- 92

Sura Ya Nane: MAZOEZI MCHANGANYIKO ---------- 99

Sura Ya Tisa: MTIHANI WA KUMALIZA DARAJA LA KWANZA ---------- 118

WASIFU WA MWANDISHI ---------- 130

VITABU VYA REJEA ---------- 132

# WAKFU MAALUM

Kwa heshima ya Prof. Fr. Charles Nyamiti;

Nimeandika kitabu hiki kwa heshima na kumbukumbu ya mwalimu wangu wa kwanza wa muziki, **marehemu Prof. Fr. Charles Nyamiti**, bila shaka, yeye ndiye chimbuko la safari yangu katika tasnia ya muziki, na daima nitajivunia kuwa mmoja wa wanafunzi wake.

Nakumbuka ilivyokuwa changamoto kubwa mwanzoni kujifunza lugha ya muziki, lakini kwa upeo wake mkubwa na mbinu zake rahisi za kufundisha, alinifanya nipende muziki kwa dhati. Ustadi wake haukuwa tu katika kufundisha, bali pia katika kuhamasisha na kukuza vipaji. Kutokana na mwongozo wake, muziki umebaki kuwa sehemu muhimu ya maisha yangu hadi leo.

Nitaendelea kumkumbuka na kumuombea daima apate pumziko la amani milele. Urithi wake utaishi kupitia kazi zake na wanafunzi wake aliowainua.

# SHUKRANI


- ♪ Namshukuru Mungu mwingi wa rehema, anayenijalia zawadi ya uhai, aliyenipa akili na kipaji hata nikaweza kuandika kitabu hiki ili kiweze kutoa mwanga na msingi imara kwa yeyote anayependa kusoma na kujifunza muziki kwa hatua.

- ♪ Namshukuru kwa dhati kabisa ndugu yangu Dkt. Jacob Martin Mulikuza, aliyenishauri na kunihimiza nianze mara moja kuandika kitabu hiki; hakika bila ushauri wake na hamasa kubwa aliyonipatia, nisingeweza kabisa kuihamisha elimu yangu ya muziki kuwa katika mfumo wa kitabu.

- ♪ Nawashukuru sana walimu wangu walioendelea kunipatia hii elimu adhimu ya muziki; kwanza kabisa Mwl. John Steven Mgandu, aliyenifundisha daraja la tatu na la nne, pili rafiki yangu wa karibu sana Mwalimu Peter Simon Haule ambaye alitumia muda wake mwingi kunifundisha na kuhakikisha nafanya mitihani ya bodi (*ABRSM*) daraja la tano na la sita na kufaulu kwa alama za juu kabisa, nadharia na vitendo.

- ♪ Namshukuru sana ndugu yangu Mwl. Peter Simon Haule ambaye alikubali kutenga muda wake na

kutumia taaluma yake na weledi mkubwa alionao katika tasnia ya muziki kuweza kuhariri kitabu changu.

- ♪ Kwa moyo wa dhati kabisa, namshukuru sana mke wangu Maria Aloyce Mtunya na familia yangu kwa ujumla, hakika wao ni faraja yangu kubwa kwa siku zote, na hasa kwa kipindi chote nilipokuwa nikiandika kitabu hiki.

**MWISHO**.

- ♪ Napenda nikushukuru kwa dhati, wewe uliyeamua kujifunza muziki kwa hatua, kwa kutumia kitabu hiki. Nina imani kubwa utapata mwanga wa kutosha katika safari yako na ndoto ulizonazo za kujifunza ili muziki uwe sehemu ya maisha yako.
- ♪ Usisite kuwasiliana nami, kwa ushauri na mapendekezo ili kwa pamoja tuweze kusaidiana na kuhakikisha tasnia ya muziki inakua zaidi ndani ya jamii yetu na katika taifa letu kwa ujumla.

Nakutakia mafanikio mema zaidi unapoanza Safari yako ya Muziki kwa kutumia kitabu hiki.

**Kasenga Michael William**
Dar-Es-Salaam, 2025

# UTANGULIZI

**Kitabu hiki** *"Anza Safari ya Kujifunza Nadharia ya Muziki Hatua ya Kwanza"*, *Mwongozo wa Mwalimu na Mwanafunzi kwa Mafunzo ya Nadharia ya Muziki Hatua ya Kwanza* Kimeandaliwa kwa lengo kubwa la kuwapatia msingi bora na imara wale wote wanaotamani kujifunza muziki hatua kwa hatua. Mwandishi anaamini kuwa, ili upate msingi mzuri wa kitu fulani, huna budi kujifunza kitu hicho kwa mtiritiko ulio sahihi ili uweze kupata msingi bora na imara.

Pamoja na lengo la kutoa msingi bora kwa hatua ya kwanza, kitabu hiki kimesheheni mambo yote muhimu kwa anayejifunza muziki hatua ya kwanza, pia kitamuongoza mwalimu kuwafundisha wanafunzi wake kwa urahisi kwa sababu mwandishi ametumia uwezo wake na elimu aliyonayo katika tasnia ya muziki kuhakikisha anakiandika kitabu hiki kwa lugha nyepesi kabisa inayoeleweka vizuri. Ndani ya kitabu hiki, kuna mifano mingi kwa kila sura na mazoezi mengi ambayo yatamsaidia mwanafunzi kufikia lengo lake na ndoto yake katika tasnia ya muziki.

*"Ukitaka uwe hodari katika jambo fulani, inakubidi uiruhusu akili yako iamue kukufanya uwe hodari, huna budi kufuata maelekezo na miongozo mbalimbali itakayokufikisha kwenye uhodari". -* ***John Steven Mgandu***